

# **Wakodishaji Wanaweza Kustahili Msaada Wa Kukabiliana na Janga**

---

**Release Date: Septemba 30, 2021**

**NEW YORK** – Msaada wa nchi wa kukabiliana na majanga si wa wamiliki wa nyumba tu. Pia, unapatikana kwa wakodishaji wanaostahili, na unaweza kushughulikia gharama kama vile fanicha, vifaa vinahusiana na kazi, urekebishaji wa gari, na vilevile gharama za kitiba na za matibabu ya meno zinazosababishwa na janga.

Wakodishaji wanaoishi katika majimbo ya **Bronx, Kings, Nassau, Queens, Richmond, Rockland, Suffolk na Westchester** waliopata uharibifu, hasara au hawawezi kuishi katika nyumba zao baada ya Kimbunga cha Ida wanaweza kustahili kupata msaada kutoka kwa FEMA na Shirika la Marekani linalosimamia Biashara Ndogo.

Ikiwa una bima ya mkodishaji, kwanza pigia mhudumu wako wa bima ili kusajili dai. Kisha jiandikishe na FEMA. Ikiwa una bima ni lazima uandae habari kwa FEMA kutoka kwa mhudumu wako wa bima, ambayo inaweza kutia ndani **mkataba au kutokubaliana**.

Msaada wa FEMA wa kukodisha umenuiwa kushughulikia kodi ya kila mwezi na gharama za huduma muhimu (k.v., gesi, umeme na maji). Misaada ya FEMA pia inaweza kutumika kwa amana za usalama lakini si kwa simu, nyaya au huduma za intaneti.

Wakodishaji lazima waweze kudhibitisha kwamba waliishi katika makao yaliyoharibiwa na janga kabla ya kupokea msaada wa Makao ya FEMA na aina nyingine za Misaada ya Mahitaji Mengine ya FEMA (k.v., ya mali ya kibinagsi na gharama za kuhama na kuhifadhi).

Ili kudhibitisha kwamba aliishi katika nyumba hiyo, nusura anaweza kuwasilisha kwa FEMA: makubaliano ya kukodi au kuishi, risiti za kodi, gharama za huduma, stimenti ya mfanyakanyabiashara, stimenti ya ofisa wa umma, kadi za utambulisho, stakabadhi za shirika la ruzuku ya jamii, stakabadhi za shule katika



**FEMA**

Page 1 of 3

eneo, stakabadhi za udhamini wa nchi au jimbo, usajili wa gari, shuhuda ya mahali unapoishi au stakabadhi zingine za mahakamani na stakabadhi za kuegesha makao yanayoweza kuhamishwa. Wataalamu wa laini ya msaada ya FEMA ya 800-621-3362 (711/VRS) wanaweza kuandaa habari zaidi kuhusu stakabadhi zinazokubalika, tarehe zao na maelezo.

Wakodishaji wanaweza kutumwa kwenye shirika la Marekani linalosimamia Biashara Ndogo, ambalo huandaa mikopo ya janga yenye riba ya chini kwa manusura. Mikopo ya SBA inaweza kusaidia kulipia hasara zisizosimamiwa na bima. Wakodishaji wanaweza kuomba mikopo ya hadi dola 40,000 ili kurekebisha au kununua vitu vya nyumba vilivyoaribiwa kutia ndani mavazi, fanicha, vifaa na vitu vingine vya kibinafsi kutia ndani magari. Wale ambaa hawastahili mikopo ya SBA wanaweza kurudishwa kwa programu ya msaada wa Mahitaji Mengine ya FEMA.

Ikiwa umetumwa kwa SBA, unapaswa kujaza na kuwasilisha ombi. Ikiwa ombi lako limekubaliwa, si lazima ukubali mkopo lakini kukosa kuwasilisha ombi kunaweza kukufanya usistahili kupata msaada mwingine wa FEMA ambaa huenda ukapata.

Kuna njia kadhaa za kuijandikisha kwa ajilii ya msaada wa FEMA:

- Tembelea [DisasterAssistance.gov](#), tumia programu ya FEMA ya simu ya mkononi au pigia laini ya Msaada ya FEMA ya 800-621-3362 (711/VRS). Laini zinatumika kati ya saa mbili asubuhi hadi saa moja jioni siku saba za wiki, na wahudumu wanaweza kukuunganisha na mtaalamu anayezungumza lugha yako. Ikiwa unatumia huduma ya kupeperusha kama vile huduma ya kupeperusha video, huduma za kutoa maelezo ya simu au zingine, wape FEMA namba ya huduma hiyo.

FEMA pia imefungua Vituo vya Kurejesha Hali Baada ya Janga ambapo unaweza kukutana uso kwa uso na wafanyakazi wa FEMA na wawakilishi wa mashirika mengine ya nchi na jimbo ambaa wanaweza kuandaa habari kuhusu msaada wa janga unaoweza kuupata. Ili kupata kituo cha kurejesha hali kilicho karibu nawe, tembelea [DRC Locator \(fema.gov\)](#).

Ili kujaza ombi la mkopo wa SBA, tembelea tovuti salama ya SBA kwa <https://DisasterLoanAssistance.sba.gov>. Pia, unaweza kutuma barua pepe kwa



**FEMA**

Page 2 of 3

[DisasterCustomerService@SBA.gov](mailto:DisasterCustomerService@SBA.gov) au pigia Kituo cha Huduma za Wateja cha SBA kwa 800-659-2955 ili kupata habari zaidi.

Siku ya mwisho ya kujaza ombi la msaada wa FEMA ni **Ijumaa, Nov. 5.**

Kwa habari zaidi mtandaoni na vijitabu vinavyoweza kupakuliwa vyta FEMA, tembelea [DisasterAssistance.gov](https://www.DisasterAssistance.gov) na ubonyeza "Information."

Ili kutumwa kwa mashirika yanayotegemeza huduma hususa za jamii, wasiliana na kituo kilicho karibu zaidi na wewe cha 211Counts kwa

<https://www.211nys.org/contact-us> au piga 211. Kwa waakazi wa Jiji la New York, piga 311.

Ili kupata habari za karibuni zaidi za New York kuhusu juhudini za kurejesha hali baada ya Kimbunga cha Ida, tembelea [www.fema.gov/disaster/4615](http://www.fema.gov/disaster/4615). Tufuate kwa Twitter kwa [twitter.com/femaregion2](https://twitter.com/femaregion2) na [www.facebook.com/fema](https://www.facebook.com/fema).



**FEMA**

Page 3 of 3